



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UAMUZI WA RUFAA ZA  
WAGOMBEA UDIWANI**

**Dodoma, 06 Desemba, 2022**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha leo tarehe 6 Desemba, 2022 imepitia, imechambua na kuzifanyia uamuzi rufaa tatu za wagombea Udiwani zilizowasilishwa kwa Tume.

Rufaa hizo zimewasilishwa kufuatia baadhi ya wagombea Udiwani kutoridhika na maamuzi ya Wasimamizi wa Uchaguzi kufuatia mapingamizi yaliyoweka katika zoezi la uteuzi uliofanyika tarehe 30 Novemba, 2022 katika Kata 12 za Tanzania Bara.

Katika kikao hicho, Tume imezipitia, kuchambua na kuzifanyia uamuzi jumla ya rufaa **Tatu** za wagombea Udiwani na kutoa maamuzi yafuatayo:-

- i. Imekubali rufaa ya Ndugu Joseph Yunja Machiya kupitia ACT-WAZALENDO na kumrejeshwa katika orodha ya wagombea wa Udiwani katika Kata ya Mwamalili, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.
- ii. Imekubali rufaa ya Ndugu Vitali Mathias Maembe kupitia ACT-WAZALENDO na kumrejeshwa katika orodha ya wagombea wa Udiwani katika Kata ya Dunda, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.
- iii. Imekubali rufaa ya Ndugu Samwel Azaria Mnyella kupitia NCCR-MAGEUZI na kumrejeshwa katika orodha ya wagombea wa Udiwani katika Kata ya Majohe, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Tume imefikia maamuzi hayo kwa kuzingatia Kifungu cha 44 (5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 kikisomwa pamoja na kanuni ya 29(1), (2) na 30 (4) za Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani), 2020 ambavyo vinatoa fursa kwa wagombea Udiwani kukata rufaa wanapokuwa hawajaridhika na uamuzi wa Wasimamizi wa Uchaguzi kutokana na pingamizi zilizowasilishwa na vinaipa Tume mamlaka ya kukubali au kutengua uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi.

Tume inatumia nafasi hii kuwapongeza wagombea na vyama vyao vya siasa ambao walifuata taratibu za kisheria katika kudai haki zao, kuhakikisha wanatimiza malengo yao ya kushiriki katika uchaguzi huu mdogo ili kupata ridhaa ya wananchi na kuwa viongozi katika kata husika.

Aidha Tume inaendelea kuwakumbusha wadau wote wa uchaguzi kuzingatia na kufuata njia sahihi zilizowekwa kisheria, ili kutatua changamoto zozote zinazojitokeza katika kipindi hiki cha kampeni kuelekea uchaguzi huu mdogo, ikiwemo kufuata maadili ya uchaguzi ambayo vyama vyote vya siasa viliridhia kuyafuata wakati wa uchaguzi.

Kwa upande mwingine Tume pia inawakumbusha wasimamizi na watendaji wote wa uchaguzi katika maeneo husika kuzingatia sheria, kanuni, taratibu, maelekezo ya Tume katika kuendesha na kusimamia uchaguzi huu.

Uchaguzi huu Mdogo wa Udiwani unafanyika katika kata Saba ambazo ni Majohe (Dar es Salaam CC) Dar es Salaam, Mndumbwe (Tandahimba DC) Mtwara, Njombe Mjini (Njombe TC) Njombe, Dunda (Bagamoyo DC) Pwani, Mwamalili (Shinyanga MC) Shinyanga, Mnyanjani (Tanga CC) Tanga, na Vibaoni (Handeni DC) Tanga.

Uchaguzi huo utafanyika sambamba na uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Amani, Wilaya ya Mjini, Zanzibar siku ya **Jumamosi, tarehe 17 Disemba, 2022.**

Upigaji Kura utafanyika katika vituo vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Vituo vitafunguliwa saa moja kamili (1:00) asubuhi na kufungwa saa kumi kamili (10:00) jioni.

Tume inatoa rai kwa wananchi wote wa maeneo hayo kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura.



Dkt. Wilson Mahera Charles  
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**